JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

ISO 9001:2015 CERTIFIED

**KATIKA KAMATI YA MAUDHUI YA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA, DAR ES SALAAM**

**SHAURI NA. 14- 2021/2022**

**DHIDI YA**

**MILLARD AYO TELEVISION**

**UAMUZI**

**UAMUZI WA KAMATI YA MAUDHUI KUHUSU MASHTAKA YA UKIUKAJI WA KANUNI ZA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI NA POSTA (MAUDHUI MTANDAONI), 2020**


## 1.0 MAELEZO KUHUSU UKIUKAJI WA KANUNI

1.1 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ilitoa leseni ya kutoa maudhui mtandaoni kwa **MILLARD AYO TELEVISION**, kwa ajili ya kuchapisha na kutangaza habari mbali mbali mitandaoni.

1.2 Kwa mujibu wa Kanuni ya 4 ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui Mtandaoni), 2020, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ina jukumu la kutunza kumbukumbu za watoa huduma wote wa maudhui mtandaoni pamoja na kuchukua hatua stahiki za kisheria dhidi ya mtoa huduma yo yote wa maudhui mitandaoni atakayekiuka Kanuni za Maudhui Mtandaoni au sheria nyingine.

1.3 Tarehe 26 Julai, 2022, Kituo cha **MILLARD AYO TELEVISION** kilirusha na kuonesha picha za kutisha za miili ya watoto wa Shule ya Msingi ya King David waliofariki dunia katika ajali mbaya ya basi la shule iliyotokea eneo la Mjimwema, nje kidogo ya mji wa Mtwara. Kituo cha **MILLARD AYO TELEVISION** kilitoa taarifa kuhusu ajali hiyo na kuonesha picha ya miili ya watoto hao wazi wazi

kinyume na Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui Mtandaoni), 2020 na Maadili ya Uandishi na Utangazaji wa Habari. Picha za tukio la gari lililoanguka pamoja na miili ya watoto waliofariki dunia iliyooneshwa wazi ni kama ifuatavyo:




1.4 **MILLARD AYO TELEVISION** walirusha picha hizo za watoto waliofariki dunia katika ajali hiyo bila kuzingatia Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui Mtandaoni), 2020 ambazo zinamtaka mtoa huduma za utangazaji azingatie Weledi na Maadili ya Uandishi wa Habari katika kuweka maudhui mtandaoni na kuhakikisha maudhui yake hayaleti usumbufu wa kisaikolojia kwa watazamaji wake au kusababisha woga/wasiwasi. Aidha, Kanuni na Maadili ya Uandishi na Utangazaji yanamtaka mtoa huduma za utangazaji kutoweka au kuonesha kwa uwazi picha za majeruhi waliopata ajali mbaya au miili ya watu waliofariki dunia kwa ajali au picha za watu waliouwawa.

## 2.0 KANUNI ZILIZOKIUKWA

2.1 Kwa kitendo cha kuweka wazi na kurusha picha za miili ya watoto waliofariki dunia, **MILLARD AYO TELEVISION** imekiuka Kanuni ya 9 (a) ,12 (a), 16 (1)) (2) pamoja na Aya ya 3 (j) ya Jedwali la Tatu katika Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui Mtandaoni) 2020, ambazo zinasomeka kama ifuatavyo:

> 9. A licensee shall comply with all the terms and conditions of the licence and observe the following:
>
> (a)ensure that online content is safe, secure and does not contravene the provisions of any written law.
>
> 12. The online news and current affairs licensee shall-
>
> (a) adhere to journalism ethics, professionalism and local content requirements;
>
> 16. (1) A person shall not publish any prohibited content as set out in the Third Schedule.
>
> (2) A person shall not render, possess or distribute technology, program, application or any other related thing that allows or helps users to have access to prohibited content.
>
> **THIRD SCHEDULE**
>
> **3. Public Security, Violence and National Safety**
>
> (j) content that portrays sadistic practices and torture, explicit and excessive imageries of injury and aggression, and of blood or scenes of executions or of people clearly being killed.

## 3.0 WITO WA KUTOA MAELEZO YA UTETEZI.

3.1 Tarehe 29 Julai, 2022, Kamati ya Maudhui ilikiandikia Kituo cha **MILLARD AYO TELEVISION,** wito wa kuwasilisha utetezi wa maandishi na kufika mbele ya Kamati ya Maudhui tarehe 01 Agosti, 2022, Saa 08:00 Mchana ili kujieleza kwa nini hatua za kisheria zisichukuliwe dhidi yake kwa kukiuka Kanuni za Maudhui Mtandaoni, 2020 kama zilivyoainishwa hapo juu.

3.2 Tarehe 01 Agosti, 2022, **MILLARD AYO TELEVISION** iliwasilisha utetezi wake wa maandishi, uliosainiwa na **Millard Ayo,** Mkurugenzi Mtendaji. Pia, **MILLARD AYO TELEVISION**, ikiwakilishwa na **Millard Ayo** ilifika mbele ya Kamati kutoa utetezi wake.

**4.0 KUSOMEWA MASHTAKA NA KUANGALIA MAUDHUI YA MILLARD AYO TELEVISION YANAYOTUHUMIWA.**

4.1 Kamati ya Maudhui iliusomea Uongozi wa **MILLARD AYO TELEVISION** mashtaka yake. Pia, Kamati na Uongozi huo kwa pamoja waliangalia maudhui yaliyochapishwa na Kituo hicho katika tarehe na kipindi tajwa hapo juu na kisha kuwaalika kujitetea ili kujiridhisha iwapo maudhui hayo yalikiuka Kanuni.

**5.0 UTETEZI WA MILLARD AYO TELEVISION**

5.1 Katika utetezi wao wa maandishi, **MILLARD AYO TELEVISION** walianza kwa kukiri kuchapisha maudhui yanayotuhumiwa. Walidai kuwa kilichotokea ilikuwa ni bahati mbaya kwa kuwa mwandishi alijisahau na kupandisha mtandaoni "cover" ambayo haikutakiwa kwenda. Waliendelea kudai kuwa mwandishi alikuwa akifahamu kwamba kuchapisha picha hizo ni kinyume na Kanuni na Maadili ya Uandishi wa Habari na ndio maana picha hizo zilifutwa ndani ya sekunde chache baada ya kupandishwa;

5.2 Waliomba radhi kwa kilichotokea na kuahidi kuongeza umakini zaidi kwenye kukusanya, kuchakata na uchapishaji wa taarifa zake siku zote ili kuzingatia Kanuni, Maadili ya Uandishi na Utangazaji Habari;

5.3 Walimalizia kwa kuomba utetezi wao upokelewe na Kamati. Kamati ilipokea utetezi wa maandishi wa **MILLARD AYO TELEVISION** kama Kielelezo Namba 1.

Pia, **MILLARD AYO TELEVISION** ilitoa utetezi wake kwa mdomo kama ifuatavyo:

5.4 **Millard Ayo** alisema kuwa picha inayotuhumiwa aliipandisha mtandaoni yeye mwenyewe. Alidai kuwa lililotokea ni kosa la kibinadamu na ndio maana aliifuta picha hiyo ndani ya muda mfupi sana baada ya kuipandisha mtandaoni. Alidai kuwa alikuwa amepokea picha nyingi kutoka kwa waandishi marafiki na kwa bahati mbaya alikosea na kupandisha mtandaoni picha mbaya inayotuhumiwa badala ya nzuri aliyokuwa ameiandaa;

5.5 Aliendelea kusema kuwa amekuwa akifanya kazi za Maudhui Mtandaoni yeye mwenyewe kwa miaka mitatu sasa ili kujiepusha na makosa. Alidai kuwa Kanuni na Maadili ya Uandishi na Utangazaji wa Habari anazifahamu vizuri na kujitahidi kuzifuata;

5.6 Aliomba radhi, na akaaihidi kujirekebisha na kwamba atakuwa tayari kupokea ushauri ili kufanya vizuri zaidi hapo baadae;

5.7 Wakati akiulizwa maswali na Kamati, alijibu kuwa hawakuomba radhi kwa watazamaji wao kwa sababu waliishusha mtandaoni picha inayotuhumiwa ndani ya muda mfupi na walidhani kuwa haikusambaa. Hata hivyo, waligundua kuwa ilisambaa kiasi kwa sababu walipokea maoni (comments) za watazamaji wao mia tatu (300) kabla hawajaiondoa mtandaoni. Alisema kuwa yupo tayari kuomba radhi. Aliishukuru Kamati kwa ushauri mzuri iliyompatia na kuahidi kuufanyia kazi.

## 6.0 TATHMINI YA KAMATI

6.1 Kamati ya Maudhui imezingatia maelezo yote ya **MILLARD AYO TELEVISION** na kubaini kuwa Kituo kimetenda kwa uzembe, kosa la kuweka wazi na kurusha/kuchapisha mtandaoni picha za miili ya watoto waliofariki katika ajali, kama walivyokiri wenyewe na kama ambavyo picha hizo zimeonekana mtandaoni. Kitendo hiki ni kinyume na Kanuni ya 9 (a) ,12 (a), 16 (1) (2), Aya ya 3 (j) ya Jedwali la Tatu katika Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui Mtandaoni) 2020 pamoja na Maadili ya Uandishi na Utangazaji wa Habari;

6.2 Kamati imeona kuwa utetezi wa **MILLARD AYO TELEVISION** kwamba alidhani maudhui hayo hayakusambaa baada ya kuyaondoa mtandaoni ndani ya muda mfupi hauna msingi wo wote kwa sababu wao wenyewe wamekiri kuwa walipokea maoni (comments) za watazamaji wao mia tatu (300) kabla ya kuyaondoa maudhui yao mtandaoni. Pia, kiuhalisia maudhui ya mtandaoni husambaa haraka sana kwa sababu watazamaji huyanakili kutoka katika chanzo chake na kuyasambaza katika kurasa nyingine mitandaoni. Hivyo, maudhui ya **MILLARD AYO TELEVISION** mtandaoni yalisambaa na kuwadhalilisha marehemu husika na hivyo kupelekea usumbufu wa kisaikolojia kwa watazamaji wake pamoja na kuwasababishia hofu, woga na wasiwasi;

6.3 Pia, Kamati ya Maudhui imebaini kwamba utetezi wa **MILLARD AYO TELEVISION** kuwa walichapisha picha hizo kwa bahati mbaya hauna mashiko yo yote kwa kuwa wanapaswa kuwa na usimamizi/uhariri makini wa maudhui yao na hivyo kutoruhusu maudhui yasiyofaa kuchapishwa mtandaoni. **MILLARD AYO TELEVISION,** kama chombo cha habari chenye watazamaji wengi mtandaoni, kina wajibu wa kuilinda jamii dhidi ya maudhui yasiyofaa na kuhakikisha kuwa utu wa binadamu unalindwa na kuheshimiwa. Pia, wanapaswa kuhakikisha kuwa Utamaduni na Maadili ya Kitanzania pamoja na Maadili ya Uandishi na Utangazaji wa Habari yanazingatiwa ipasavyo;

6.4 Kamati imejiridhisha kuwa **MILLARD AYO TELEVISION** imekosa umakini katika usimamizi kwenye utayarishaji na utangazaji wa maudhui yao mtandaoni, hivyo kusababisha ukiukaji wa Kanuni kulikowafanya watende makosa hayo.

## 7.0 MAELEKEZO YA KAMATI KWA MILLARD AYO TELEVISION

Kutokana na kosa lililobainika, Kamati inaielekeza **MILLARD AYO TELEVISION** yafuatayo:

7.1 Kuhakikisha inazingatia Misingi, Sheria, Kanuni, Maadili, Weledi, Vigezo na Viwango vya tasnia ya Uandishi na Utangazaji wa Habari katika kutayarisha/kuandaa, kusimamia, kufuatilia, kutathmini na kutangaza maudhui yao mtandaoni;

7.2 Kuwa na Bodi ya Uhariri inayoundwa na wanataaluma wa Uandishi wa Habari ili kuwasaidia katika kufanya uchambuzi na maamuzi sahihi yanayozingatia taaluma katika kazi zao;

7.3 Kuhakikisha inadumisha Utamaduni wa Kitanzania wa kuheshimu, kutunza na kulinda utu wa binadamu pamoja na heshima ya marehemu katika uwasilishaji wa maudhui yao;

7.4 Aidha Kamati ya Maudhui inasisitiza kuwa ni kosa Kisheria kupiga picha na kuonyesha au kusambaza kwenye Mitandao ya Kijamii miili ya watu waliokufa kwa ajali au kwa namna yoyote ile. Kamati itachukua hatua kali za Kisheria kwa chombo chochote cha Utangazaji au Mitandao ya Kijamii itakayochapisha na kusambaza picha za namna hiyo.

## 8.0 UAMUZI WA KAMATI

8.1 Baada ya kutafakari kwa kina utetezi wa **MILLARD AYO TELEVISION**, Kamati ya Maudhui imeridhika pasi na shaka kuwa **MILLARD AYO TELEVISION** imekiuka Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui Mtandaoni), 2020 kama ilivyoainishwa katika Tathmini ya Kamati hapo juu.

8.2 Hivyo basi, kwa mujibu wa Kanuni ya 21 (3) (a) na (b) ya Kanuni tajwa za Maudhui Mtandaoni, 2020, Kamati ya Maudhui inatoa adhabu zifuatazo kwa **MILLARD AYO TELEVISION:**

1. Inapewa Onyo;

2. Inaamuriwa kuomba radhi kwa watazamaji wake kwa siku tatu (3) mfululizo kupitia chombo chake cha Habari kilichotumika kutenda kosa hilo.

Uamuzi huu umetolewa Dar es Salaam, leo tarehe **09 Agosti, 2022**

Haki ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi huu kwenye Baraza la Ushindani wa Haki Kibiashara (Fair Competition Tribunal – FCT) iko wazi ndani ya siku 21 (ishirini na moja) kuanzia siku ya kutolewa kwa uamuzi huu.

**Uamuzi huu umesainiwa na:**

**Ndalahwa Habbi Gunze**

..............................................................

**Mwenyekiti wa Kamati ya Maudhui**

MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
20 BARABARA YA SAM NUJOMA
S. L. P. 474
14414 DAR ES SALAAM
TANZANIA

**PAMOJA NA WAJUMBE WAFUATAO WA KAMATI YA MAUDHUI:**

1. **Derek Kaitira Murusuri** ..............................

2. **Jacob Gregory Tesha** ..............................